BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

POWDER
YA MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

Wasafishaji mashuhuri wa picha za rangi za *FUJI* ulimwenguni sasa wanapatikana mjini Mombasa

Aina zote za picha za rangi zinachapishwa:

FUJI • KODAK • AGFA
SAKURA • COLOURAMA

KWA USAFISHAJI WA PICHA ZAKO ZOTE ZA RANGI HAKIKISHA UNAZITUMA KWA MITAMBO MIPYA YA KISASAS YA FUJI

Zungumza na *Riaz Alibhai* kwa simu 313589, Mombasa ama fika kwenye mitambo hiyo mipya ya *FUJI*, iliyo pakana na afisi ya *Coastweek*, gorofa ya kwanza ya jumba la Banki ya Grindlays, katika barabara ya Digo Road na Nkrumah road.

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

HEKO V.O.K.

NI JAMBO la kufurahisha sana kuona kwamba mchezo wa kwanza wa Mapambano ya Kugombania Kombe la Washindi wa Klabu za Afrika baina ya AFC Leopards na Asante Kotoko ulionyeshwa kwenye mitambo ya televisheni.

Mchezo huo ulio chezwa kwenye Kiwanja cha Kumasi Ghana ulikuwa wa kufurahisha na sisi mashabiki hapa nchini tuliona makosa ambayo yalifanywa na timu yetu pamoja na kugundua mbinu zilizoonyeshwa na wapinzani wetu.

Twaishukuru V.O.K. kwa kutuonyesha sinema hiyo lakini ajabu ni kwamba kuna mipambano mingine hatukuwahi kuonyeshwa. Natoa ombi michezo yote ambayo timu zetu zinashiriki nje zionyeshwe kwenye televisheni.

MAKOSA

Tukionyeshwa, basi sisi mashabiki tutaweza kuona makosa yetu yako wapi badala ya timu kurudi na kulalamika kuwa labda waamuzi wamewaonea na madai mengine ya kawaida yanayotolewa na maafisa wanaofuatana na timu hizo.

Twamuomba Waziri Noah Katana Ngala afanye taratibu za kuwatuma wapiga picha wetu kila timu ama timu zetu za Taifa zinaokwenda nje ili baadaye watuonyeshe sinema hizo na sisi ndio tuwe waamuzi wa kama haki ilitumika ama la!

DAVIS MUNGA
NA
BARNIE KALUME,
MOMBASA.

MWENYEKITI wa Bodi ya Shule ya Upili ya Allidinah Visram Bw. Chokwe (aliyeketi kulia) akiidhinisha kandarasi ya ujenzi wa Maktaba mpya ya Shule hiyo katika sheherehe ambapo jiwe la msingi liliwekwa kuanzisha ujenzi huo. Sherehe hiyo ilihudhuriwa na Mwalimu Mkuu Bw. Mokua (aliyeinama), Niwenyekiti wa Kamati ya Waalimu na Wazazi Bw. Waweri (aliyesimama nyuma ya Mokua), Mwenyekiti wa Chama cha Wanafunzi wa Zamani wa shule hiyo Bw. Bashir A. Bachani (akisimama nyuma ya Bw. Chokwe) na Diwani Abubakar (akimtazama Bw. Chokwe). Ujenzi huu unagharimiwa na Chama cha Wanafunzi wa Zamani wa Shule hiyo.

MSIKITI WA SWAFAA WA LAMU WAJENGWA

MSIKITI wa Swafaa uliojengwa mwaka wa 1971, Msikiti wa pili maarufu kisiwani Lamu, unafanyiwa marekebisho makubwa kwa kujengwa upya na utakapokamilika utagharimu kiasi cha Shilingi Milioni Nane Unusu 8,500,000/- *(Aripoti Abdulrahman Sheriff).*

Msikiti huo uko katika eneo la Langoni, eneo ambalo watu wa Lamu wamelibadilisha jina na kuliita Swafaa kwa heshima ya Msikiti huo. Mkao wa Muassasati Ahlil-bayt ndio unaosimamia ujenzi wa Msikiti.

Msikiti Swafaa ambao umeelekezana na mahali amabapo Mtukufu Rais Moi aliweka jiwe la Ukumbusho wa maafa ya wananchi wa Lamu walioteketewa na nyumba zao, utakuwa mkubwa kuliko yote Kisiwani.

Msemaji wa usimamizi wa ujenzi wa Swafaa aliniambia wakati wa ziara yangu ya mapumziko mjini Lamu kwamba msikiti huo utajengwa gorofa moja. Chini wataswali wanaume na juu wanawake watafanya ibada zao pamoja na kujifunza mafunzo ya Dini ya Kiislamu.

Aliongeza mwemaji huyo kwamba sehemu moja itakuwa ya kufundishia Akina Mama kushona na kufuma na hali sehemu nyingine itakuwa ya malazi kwa wanafunzi wanaotoka nje ya Lamu; wanafunzi ambao watachaguliwa bila ya ubaguzi wowote kusoma katika Chuo Kikuu.

TANZANIA

Nilipomuuliza kama kuna wanafunzi wa nje ya Kenya watakaosoma katika Chuo Kikuu hicho cha Msikiti wa Swafaa, msemaji huyo alisema huenda wakapokea wanafunzi kutoka Tanzania na sehemu nyingine za nchi jirani.

"Lakini upokeaji ama ualishi wa wanafunzi kutoka nje ya Kenya utategemea kukamilika kwa ujenzi wa msikiti", akasema na kufahamisha kuwa wanafunzi wa kutoka nje ya Lamu watapata huduma zote bure bila ya kulipa chochote. Huduma zenyewe ni masomo, malazi na chakula.

Msikiti wa zamani katika Lamu ni ule unaojulikana kama wa *Pwani* **lakini Maulidi Makubwa na kilelel cha mfululizo wa Maulidi yanayofanyka kila msikiti na kuhudhuriwa na maelfu ya Waislamu kutoka katika kila pembe ya ulimwengu hufanyika katika Msikiti maarufu wa** *Riadha.*

Maulidi makubwa ya pili hufanyika katika Msikiti wa Swafaa ambao sasa unajengwa upya. Ingawa ujenzi wote wa Msikiti utakuwa haujakamilika wakati wa Mwezi wa Mfungo Sita, wasimamizi wa maulidi katika msikiti huo alisema, "Kama ada yetu, tutafanya maulidi Msikitini".

Mji wa Lamu una wakazi wapatao 10,000 ambao karibu asilimia 98 ya wakazi hao ni Waislamu. Mji huo una jumla ya Misikiti yapatayo 25 yakiwemo manne yaliyojengwa Sheila umbali wa Kilomita 2 kutoka Kisiwa cha kihistoria cha Lamu.

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA MSHINDI WA PILI NA WATATU ATAPATA ZAWADI YA FLANA YA FARUCCI

CROSSWORD No. 219

KWENDA KULIA:

1. Msimamizi wa wafanyi-kazi fulani. 6. Katika ua. 8. Mnyama adui wa kuku. 9. Pande la chungu kilichovunjika. 11. Jina la kike. 13. Aina ya ndege kama njiwa. 15. Kiungo cha maneno. 16. Chama chetu cha Kenya. 17. Imalizike. 18. Chagua. 19. Kwama, saki.

KWENDA CHINI:

1. Mmea wa matunda. 2. Ua la mtoni au katika ziwa. 3. Post Office. 4. Jumla ya michezo yote ya mazoezi ya viungo vya mwili. 5. Jina la kikikuyu. 7. Itangulize. 10. Afrika Masharika, 12. Jina la kigiriama. 14. Teketea. 16. Wingi wa ukuta.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 218

KWENDA KULIA: 1. MAGARI, 4. UK, 6. KUNGWAA, 8. LAMI, 9 TWAZUA, 12. IANA, 14. NA, 15. KIKOI, 16. DUNI, 17. KAA, 18. UKUNI. *KWENDA CHINI:* 1. MAKUTI, 2. ANGAZA, 3. ILALA, 5. KILINDINI, 7 AA, 10. WANDA, 11. ANAUA, 13. UKUU, 15. KIU.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 219

1. BI. JEDIDAH WAMBUI M. Sanduku La Posta 84216, Mombasa. 2. BI. REHEMA T. MASHA. Sanduku La Posta 93404, Mombasa. 3. BERTINA KALE KIAGO, Sanduku La Posta 87294, Mombasa.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Kila baada ya wiki mbili, Mshindi wa kwanza atapata viatu maridadi vya Farucci; wa pili atapata 'Bint El-Sudan-Gift Pack' na watatu atajinyakulia flana ya Farucci. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri *COASTWEEK*, S. L. P. 87270, Mombasa. Mwisho wa kutuma Majibu na jumatano, **October 16,1985** saa, nne asubuhi.



JINA...

SANDUKU LA POSTA.........................

....

MWENYEKITI wa Baraza la Lamu, Diwani Ali Mahrus (kulia) akisikiliza kwa makini kisa cha "Sayyidina Hussein" wakati wa kuadhimisha siku ya "Hussein Day" iliyofanyika katika Msikiti unaojengwa wa SWAFAA huko kisiwani Lamu.

PICHA: ABDULRAHMAN SHERIFF

FURAHA TELE KWA GOR MAHIA

TWACHUKUA fursa hii kutoa furaha zetu kwa wachezaji sita wa timu ya Gor Mahia kufungiliwa baada ya kukatazwa kucheza soka la hali ya juu kwa muda wa mwaka mzima.

Wachezaji hao, Abbas Magongo, George Onyango, George Otieno Solo, Peter Otieno Bassanga, Abbey Nassur na George Otieno Vigo wameshamaliza vifungo vyao na sasa wako huru kuonyesha mbinu zao.

Wachezaji hao sita wote ni wenye maarifu ya hali ya juu ya kulipeta soka na bila shaka sasa timu yetu ya Harambee Stars itazidi kuwa ngumu ikiwa baadhi yao watateuliwa kuchezea.

Natoa shukrani kwa vijana hao kustahamili kwa kipindi chote cha mwaka nikiwaambia wazidi kufanya biddi ili waiwezeshe timu yao ya Gor Mahia izidi kupanda ngazi ya Ligi ya Taifa.

TOM CHIKA
NA
JOSEPH KOTUGA,
MOMBASA.